

HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

TAARIFA YA MAENDELEO YA KILIMO DIVISHENI YA KILIMO MJINI

1. UTANGULIZI

Halmashauri ya Jiji la Dodoma ina jumlaya kata 41 zinazojihusisha na shughuli za kilimo na mifugo. Maafisa ugani wanaotua huduma kwa wakulima na wafugaji ni 80 ambapo 49 ni maafisa ugani mifugo, 28 ni maafisa ugani kilimo na watatu (3) ni maafisa uvuvi ambao baadhi wanafanya kazi ofisi kuu na walio wengi hufanya kazi katika kata.

MALENGO YA KILIMO

Malengo ya kilimo yanayotarajiwa kufikiwa Katika msimu wa kilimo 2022/2023, ni hekta 21,335 kwa mazao ya chakula, hekta 3,815 mazao jamii ya kunde, hekta 18,588 mazao ya biashara na hekta 484 za mazao ya mboga na matunda kama inavyoonekana katika jedwali hapa namba 2.

Jedwali Na. 2 MALENGO NA UTEKELEZAJI WA KILIMO KWA MSIMU WA 2022/2023

| MALENGO | | | |
|-------------------------------|-------------------------|------|----------------------------|
| Mazao | Eneo litakalolimwa (Ha) | Tija | Matarajio ya mavuno (Tani) |
| MAZAO YA CHAKULA | | | |
| MAZAO JAMII YA WANGA | | | |
| Mtama | 1,102 | 1.5 | 1,653 |
| Uwele | 17,314 | 1.3 | 25,971 |
| Mahindi | 515 | 1.5 | 773 |
| Mpunga | 19 | 2.5 | 48 |
| Muhogo | 876 | 6 | 5,390 |
| Viazi vitamu | 1,509 | 5 | 7,545 |
| Jumla Ndogo | 21,335 | | 41,380 |
| MAZAO JAMII YA MIKUNDE | | | |
| Kunde | 1,410 | 1.3 | 1,942 |
| Njugu | 2,405 | 1.8 | 4,329 |
| Jumla Ndogo | 3,815 | | 6,271 |
| MAZAO YA BIASHARA | | | |
| Karanga | 6,780 | 1.5 | 10,170 |
| Alizeti | 4,812 | 1.5 | 7,218 |

| | | | |
|------------------------------|---------------|----|---------------|
| Zabibu | 1,350 | 10 | 13,500 |
| Jumla Ndogo | 18,588 | | 28,664 |
| MBOGAMBOGA NA MATUNDA | | | |
| Nyanya | 225 | 20 | 4500 |
| Karoti | 27 | 10 | 270 |
| Pilipili hoho | 55 | 10 | 550 |
| Vitunguu | 65 | 20 | 1300 |
| Tikiti | 20 | 30 | 600 |
| Papai | 79 | 20 | 1580 |
| Chinese | 15 | 5 | 75 |
| Jumla Ndogo | 486 | | 8875 |
| JUMLA KUU | 44,224 | | 85,190 |

MAFANIKIO

- 1) Kutoa mafunzo ya njia bora za uzalishaji wa zabibu kwa wakulima 500 wa zabibu na maafisa ugani 25 walipata mafunzo yaliyotolewa na TARI-Makutopora, Aidha, maafisa ugani 3 waliwezesha kwenda nchini Afrika Kusini kuhudhuria mafunzo ya uzalishaji wa zabibu yaliyafadhiliwa na Halmahauri ya Jiji la Dodoma.
- 2) Uzalishaji wa miche bora ya zabibu ambapo jumla ya miche 44,506 ilizalishwa na iligawiwa kwa wakulima bure
- 3) Ukarabati wa Bwawa la Ipala, hadi kufikia sasa kiasi cha shilingi 10,000,000 zimetumika kwa kazi hiyo na ukarabati unaendelea. Bwawa hili linauwezo wa kuhifadhi maji lita miioni 1.5
- 4) Kutoa mafunzo kwa wakulima kupitia maonesho ya wakulima Nanenane kwa wiki ya kuelekea siku ya wakulima Nanenane ambapo wakulima 1865 walipata elimu hiyo
- 5) Kuwezesha wakulima kupata mbegu za ruzuku za alizeti ambapo kiasi cha tani 35 ziliuzwa kwa msimu 2021/2022 na kiasi cha tani 5 zimeuzwa kwa wakulima msimu 2022/2023. Ruzuku hii ya mbegu za alizeti imesaidia kupungua kwa bei ya mafuta ya alizeti kutoka shilingi 9,000 kwa lita hadi shilingi 4,500 kwa lita.
- 6) Kuwezesha upatikanaji wa mbolea ya ruzuku kwa kuwasajili wakulima wapatao 10, 270 ambao wanaweza kupata mbolea hiyo ya ruzuku kwa wakala aliyesajiliwa kwa bei ya shilingi 70,000 badala ya shilingi 140,000.
- 7) Kuwezesha uanzishwaji wa mashamba darasa ya alizeti na karanga ambapo kwa msimu 2021/2022 mashamba darasa 30 yalianzishwa na msimu 2022/2023 mashamba darasa 35 yameanzishwa. Aidha, Halmashauri imeanzisha shamba darasa la zabibu katika kata ya msalato
- 8) Kampeni za kilimo zimefanyika na kuwafikia wakulima katika kata na mitaaa, idadi wa wakulima waliofikiwa wanakadiriwa kuwa 12200 ikilingaishwa na mwaka jana ambapo wakulima waliofikiwa wanakadiriwa kuwa 8300

- 9) Usambazaji wa viuatilifu ambapo kwa msimu wa kilimo 2021/2022 ofisi ilipokea lita 500 za sumu ya kuuu kisumbufu cha mahindi (*fall army worm*)
- 10) Ofisi ilipokea vitendea kazi kwa maafisa ugani ikiwa ni seti ya makoti ya mvua, bomba la kupuliza sumu, gamboot kwa ajili ya kila afisa kilimo pamoja na pikipiki 25.